

# Taarifa kuhusu sheria mpya ya Victoria ya afya ya akili na ustawi

Swahili | Kiswahili

OFFICIAL

## Taarifa kuhusu sheria mpya ya Victoria ya afya ya akili na ustawi

Karatasi hii ina maelezo ya kukusaidia kuelewa sheria mpya Ya Victoria ya afya ya akili na ustawi (*Sheria ya Afya ya Akili na Ustawi wa 2022*).

Sheria mpya inatokana na haki za binadamu. Inalenga:

- kusaidia watu kuwa na afya nzuri ya akili
- kulinda watu ambao wana magonjwa ya akili
- kusaidia familia na walezi wa watu wenye magonjwa ya akili.

Sheria mpya ina kanuni za kuhakikisha huduma za afya ya akili na ustawi ni salama kwa kila mtu. Hii inamaanisha kuwa ni jumuishi na zinapatikana.

Kanuni hizi zinasema huduma za afya ya akili lazima ziheshimu watu wote katika jamii, ikiwa ni pamoja na watu kutoka tamaduni tofauti, vikundi vya lugha na asili za imani.

## Taarifa ya haki

Sheria mpya inasema mtu lazima apewe taarifa ya haki ikiwa anapata usaidizi wa afya yake ya akili hospitalini.

Taarifa ya haki ni hati inayoelezea haki za kisheria za mtu. Wafanyakazi katika hospitali lazima wamsaidie mtu kuelewa taarifa ya haki.

Taarifa ya haki inatafsiriwa katika lugha za jamii na inapatikana kwenye tovuti ya Idara ya Afya kwenye [www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act](http://www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act)

## Taarifa ya mapema ya upendeleo

Taarifa ya mapema ya mapendeleo ni wakati mtu anaandika kile anachotaka na asichotaka katika matibabu na utunzaji wa afya ya akili.

Taarifa ya mapema ya mapendeleo inaweza kusema jinsi mtu anataka usaidizi ikiwa anapata matibabu ya lazima. Kwa mfano, wanaweza kusema hawataki dawa fulani.

Wafanyakazi lazima wajaribu kufanya kile kilichomo kwenye taarifa. Ikiwa wafanyakazi hawafanyi kilichomo kwenye taarifa, lazima waandike sababu.

Mtu anaweza kutoa taarifa ya mapema ya mapendeleo wakati wowote.

## Msaидиzi аliyeteuliwa

Msaидиzi аliyeteuliwa ni mtu ambaye mtu huchagua kumsaidia ikiwa wana matibabu ya lazima.

Msaидиzi аliyeteuliwa anaweza kumsaidia mtu:

- kufanya maamuzi kuhusu matibabu na matunzo ya afya ya akili
- kuwaambia madaktari kile mtu huyo anataka.

Mtu lazima aandike anayemtaka kama mtu аliyeteuliwa, na yeye lazima akubali kuwa msaидиzi аliyeteuliwa.

## Utetezi usio wa kisheria

Kuna huduma inayoitwa huduma isiyo ya kisheria ya utetezi wa afya ya akili.

Utetezi usio wa kisheria unamaanisha kupata usaидиzi kutoka kwa mtu ambaye si mwanasheria. Mtu huyu anaitwa wakili.

Ikiwa mtu anapata matibabu ya lazima, lazima apewe msaada kutoka kwa wakili. Mtu anaweza kusema hapana ikiwa hataki wakili.

Jina la huduma hii ni Utetezi Huru wa Afya ya Akili (IMHA).

## Tume ya Afya ya Akili na Ustawi

Tume mpya ya Afya ya Akili na Ustawi husaidia kuhakikisha kuwa huduma za afya ya akili ziko salama na zinapatikana kwa wote.

Ikiwa mtu hafurahii huduma ya afya ya akili na ustawi, anaweza kuiambia Tume. Tume itasikiliza na kujaribu kutafuta suluhu.

## Je, taarifa hutumika na kushirikiwa vipi?

Sheria mpya inasema huduma za afya ya akili na ustawi zinaweza kushiriki habari na watu wengine

- ikiwa mtu anasema ndiyo
- au wakati mwингine kuweka mtu salama na vizuri.

Chini ya sheria mpya, maelezo yanaweza kushirikiwa na huduma zingine ili kuwapa watu usaидиzi bora zaidi.

Hii inaweza kuwa

- huduma za makazi
- huduma za madawa ya kulevya na pombe.

Mtu anaweza kuchagua ikiwa anataka kushiriki habari na huduma zingine.

Taarifa pia inaweza kushirikiwa na huduma ya ambulensi katika dharura.

## Ninaweza kupata wapi habari zaidi?

Kwa habari iliyopasishwa zaidi tafadhalu tembelea ukurasa wa [sheria-ya-afya-ya-akili-na-ustawi <https://www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act>](https://www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act) kwenye tovuti ya Idara ya Afya ya Victoria.

Ili kupokea hati hii katika muundo mwингine wa barua pepe [<mhwa@health.vic.gov.au>](mailto:mhwa@health.vic.gov.au).

Imeidhinishwa na kuchapishwa na Serikali ya Victoria, 1 Treasury Place, Melbourne.

© Jimbo la Victoria, Australia, Idara ya Afya, Agosti 2023.

ISBN 978-1-76131-224-3 (mtandaoni/PDF/Word)

Inapatikana kwenye tovuti [Sheria ya Afya ya Akili na Ustawi](https://www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act) <<https://www.health.vic.gov.au/mental-health-and-wellbeing-act>>